Mpendwa baada ya kusoma umeona, yapo maeneo ambayo shetani amekudanganya kwa mbinu na mikakati yake, ili uende Jehanamu. Amekupofusha macho na kuziba masikio yako ya ndani ili usiliamini Neno hili la Mungu, kwakua anajua wazi chanzo cha imani ni kusikia na kusikia huja kwa NENO LA KRISTO (Warumi 10:17).

Tambua, huwezi kumlaumu Mungu kwa kuchelewa kwako kuokoka. “Kwa kuwa Mungu hapendi mtu yeyote apotee, anapenda kila mmoja aokoke. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanaye wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele (Yoh 3:16, Rum 5:8)”.

Wala huwezi kusema sikuonywa, kwakuwa Mungu hufikisha ujumbe wake kwa mtu ampendaye kwa njia mbalimbali, ikiwemo kipeperushi hiki ili akuokoe haraka na mikono ya Shetani. Maana Ibilisi hapendi kwenda motoni mwenyewe, Ata hakikisha anaingia na wengi kama; walevi, wazinzi, wachawi, wasio samehe, wapenda rushwa, waongo, wenye hasira, na wote wenye tabia mbaya, hawataurithi ufalme wa Mungu (Wagalatia 5:19-21). Ewe rafiki, upendwaye na Mungu, usikubali tena kunaswa kwenye mtego wa Shetani. Hivyo nakusihi umwamini **BWANA YESU** sasa hivi kwa sala hii, ili ayabadili maisha yako kabisa;

***Tamka kwa IMANI...*** *“Baba Mungu katika Jina la Yesu Kristo. Asante kwa kunipenda na Yesu Kristo kufa msalabani kwa ajili yangu, ili aniokoe na dhambi zangu. Ninampinga shetani ndani ya maisha yangu leo. Ninatubu dhambi zangu zote na ninakukubali Bwana Yesu uwe mwokozi na Bwana wa maisha yangu. Nisafishe kwa DAMU YAKO iliyomwagika msalabani, Unijaze Roho wako Mtakatifu leo ili aniongoze kwenye kweli yote. Asante Yesu kwa kuniokoa. AMEN”.*

**Kwa msaada wa kiroho, usisite kutafuta Kanisa la Kiroho, la Kikristo ujitambulishe na ukasali huko ili upate kukua kiroho.** (Waebrania 10:24-25, 2Timotheo 3:16-17, 1Petro 2:1-3, Ufunuo 3:5).

**INASAMBAZWA NA**

JINA: TAG MWENGE CHRISTIAN CENTRE

ANUANI : IDARA YA UINJILISTI- +255 713 250 034

ROMMEDIA GOSPEL TRACTS_31126_+255 713 310 721

# MAPAMBANO



Mkutano ulikuwa karibu sana kumalizika. Wajumbe wengi walionyesha kumkumbusha Kinara kuwa ni wakati wa kufunga mkutano. Wengine walianza kusinzia, mara saa ya ukutani ikalia, saa nane usiku! Mkutano ulikuwa umechukua masaa manane na ulikuwa ni wa kuweka mikakati dhidi ya mwanadamu. Maeneo yote ya msingi yaliwakilishwa na majemedari wao wakuu.

Jemedari ULEVI na vibaraka wake walikuwepo kikaoni, alikua ametunukiwa zawadi nyingi kuliko majemadari wote. Moja ya mbinu zilizompa sifa na ushindi ni kwa madhehebu kadhaa ya dini kushiriki kunywa pombe, vibaraka wake walibuni mbinu kali ya kuteka fikra zao kuwa; biblia inasema kunywa pombe si vibaya ila wanywe kidogo. Waliwapa pia mbinu za kufundisha kuhusu pombe bila kuhatarisha ufalme wao wa giza. Hivyo basi waliwafanya waamini kuwa wanaweza kunywea nyumbani au dukani ili mradi tu pamesitirika. Kati ya majemadari waliosifiwa sana kwenye huo mkutano wa mwaka, ni pepo RUSHWA na vibaraka wake. Maana walibuni mbinu nyingi kama; kudhoofisha huduma katika jamii ili watu watoe rushwa, ugumu wa kupata haki, kuhujumu mali ya umma n.k. Ulikuwa pia umezuka ubishano wa nani zaidi mwaka huu kati ya pepo UBINAFSI na pepo USAGAJI, pepo ubinafsi aliwachochea watu zaidi kuwa wabinafsi wasiojali wengine na huyu USAGAJI akaona yeye ndiye anastahili sifa kwa kufanya kazi kubwa.

Pepo chuki bin Uhasama naye aliombwa na wajumbe awe mwangalifu kidogo kwani anapogonganisha nchi kama zile zinazotoa mafuta, anafanya hali ya maisha kuwa ngumu mno na watu kumgeukia Mungu. Hata Hivyo hilo halikuthibitishwa kitakwimu, maana wengine walikua na maoni tofauti kuwa, ugumu wa maisha unaongeza vitendo vya hujuma, hivyo kuzidisha hesabu ya WANAJEHANAMU.

Ndipo ghafla! mwenyekiti akasimama kweye meza na wajumbe wote wakakaa kimya. Jambo hilo lilileta mstuko, maana ilikuwa lifanyike dakika za mwisho, na lilikuwa jambo dhahiri kuwa mkuu wa majeshi yote ya giza atakaribishwa mwishoni kufunga mkutano huu wa mwaka. Na siyo kawaida yake kuhudhuria, huwa anapeleka mwakilishi tu, na kama akihudhuria, ujue basi kuna jambo muhimu la kusema au kuna mabadiliko ya kiuongozi.

Basi kila jemadari na vibaraka wake walisimama, huku pumzi zikiwatoka na majasho yakiwatiririka kwa hofu, na baada ya kupiga saluti wakamngojea mkuu wao atoe amri ya kukaa. Baada ya amri hiyo kutekelezwa, akaanza kwa kusema: “Ndugu wajumbe; kipindi hiki cha karibuni nimekuwa sina furaha hata kidogo na utendaji wenu. Ila sitachukua hatua yoyote kali kwenu, bali hatua kali zitachukuliwa kwa atakaekiuka maagano yetu ya mikakati ya leo. “Kwanza niwakumbushe jambo moja au mawili ya msingi. Ni marufuku kutaja neno “**YESU**” ndani ya kikao hiki, maana muda wetu uliobaki duniani ni mfupi mno sitaki kikao kivurugike hapa. Pili, wanaotukimbia kila siku ni wengi, hasa vijana. Mkutano uliopita tulibuni mkakati kuzuia watu wasimwamini huyo mtu (Yesu), lakini haitoshi; hata mikakati niliyoitoa hapa pia naona haitoshi.

Hapo awali mtego kama wa mafundisho yasemayo; “hakuna kuokoka duniani”, yalisaidia; lakini leo hii yameshindwa kabisa. Wengine mliwatisha kuwa kuokoka ni kubadili Dini” na takwimu zangu zinaonyesha ya kwamba maelfu wametugundua, maana kadiri INJILI inavyopamba moto, ndivyo mateka wetu wanatoroka. Nadhani mbinu ninazoona zinafaulu kidoogo, ni zile za kuwafundisha watu BIBLIA ni ngumu sana kuisoma, na mtu akiisoma hawezi kuielewa. Pia wawe wavivu wa kwenda kanisani na wakienda wasinzie wanapolisikia NENO LA MUNGU. Tamaa ya mwili, Kupenda pesa na Kutamani miujiza kuliko kumpenda Mungu, hizi zote ni silaha za kuwafanya waabudu sanamu, na Mungu wao hapendi kabisa ibada ya sanamu. Hivyo tukiwafanya wavipende watakuwa mbali na kweli ya Mungu. Nawashukuru wote waliobuni mbinu hizi na leo napenda kuwapandisha vyeo. Pepo WIVU na wasaidizi wake sasa atakuwa ni Jemadari USINGIZI, TAMAA na UZUSHI. Na Jemadari CHUKI BIN FITINA ambaye anafaulu sana karne hii kuleta ugomvi na machafuko na kuto-kusameheana. Yeye atakuwa “Field Marshall” Chuki. Tena namwomba kwa dhati azidishe ugomvi na fitina kati ya washirika wasipendane, mtu na mke wake, mtu na wazazi wake na mtu na ndugu zake ili wasisameheane na ndoa zivunjike kabisa. “Hatimaye ninamjulisha kwenu pepo kijana sana ambaye takwimu nilizo nazo zinaonyesha kuwa cheo atakachopewa leo atakimudu na mamilioni watashindwa kumfuata mtu huyu (YESU).

Huyo ndiye Pepo NGOJA KIDOGO. Amebuni mkakati ambao umeshaanza kuleta matunda mazuri. Kijana wetu ni jasiri sana. Akipata mateka hasa vijana kama yeye anawaacha waende makanisani hata kusikiliza injili, lakini atahakikisha wanavutwa na starehe, ngono na michezo ya kubashiri (kubeti); na vijana wengi sasa hivi ameshawaweka kwenye himaya yake. Mbinu yake ni kuwaambia waendelee kula raha na starehe, na wangoje kidogo mpaka baadae wakisha zeeka ndio watamrudia Mungu. Akishamaliza kazi ya kupotosha fikra zao, huwapasha habari mapepo wenzake kama vile Jemadari SAHAU na Jemadari MAUTI ili wasahau kisha wawauwe kabla ya kumkubali YESU na mwisho kwenda Jehanam kirahisi. Mbinu hii ni mpya na inafaulu mno. Msaidiane ili asiwepo mtu wa kuingia mbinguni kirahisi. Mimi nimemaliza kikao. Asiwepo atakae kiuka maagano yangu. Asanteni, tukutane kwenye uwanja wa mapambano.

Ndugu msomaji, fahamu kuwa biblia, inasema “kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili. Juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho” (Waefeso 6:12). Tumeona hapa mbinu mbalimbali ambazo shetani anazitumia katika kukufanya uwe mateka wake. Na wewe huwezi kujiokoa mwenyewe, njia pekee ya wokovu ni kumwamini Yesu tu; (Matendo 4:12).

Unaweza kusema subiri kesho, Je? Hiyo kesho ni mali yako? Mungu anasema wakati ulio- kubalika ni sasa, siyo kesho ***(2 Wakorintho 6:2).*** Una hakika gani hiyo kesho unayoingojea utaiona? Mfano, tukio la ghorofa lililodondoka pale Kariakoo Dar es salaam Novemba 2024, na kuuwa zaidi ya watu (29), tafakari kwa tukio lilivyotokea haraka vile je? ni wangapi walikuwa wamemwamini Bwana Yesu? Hapakuwa na muda wa kutubu kwenye ajali ya ghafla.